**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

OFISI YA RAIS – TAMISEMI

**NAMBA ZA SIMU:**
**Mkuu wa Shule: 0753 946150**
**Makamu Mkuu wa Shule : 0752988720**
**Blog:** https://mwlnyerere.blogspot.com
Email:mwalimunyerere17@gmail.com

**Shule Ya Sekondari Mwalimu Nyerere,**
**S. L. P. 797,**
**KAHAMA.**
**SHINYANGA.**
**Tarehe……….............**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi**
**………………………………..**
**………………………………..**
**S. L.P ………………………..**

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MWALIMU NYERERE, HALMASHAURI MSALALA, MKOA WA SHINYANGA MWAKA 2021/2022.**

Ninafurahi kukuarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na masomo ya kidato cha tano (Form V) kwa mwaka wa masomo **2021/2022** katika **shule ya Sekondari Mwalimu Nyerere iliyopo Wilaya ya Msalala, mkoa wa Shinyanga** katika tahasusi (combination) ya ………………………... Kwa muda wote mwanao atakapokuwa katika shule hii, atapaswa kushirikiana na wanafunzi wenzake, walimu na wafanyakazi wasio walimu katika kutoa mchango wake wa mawazo na vitendo ili kuleta na kudumisha sifa na maendeleo ya shule hii kwa manufaa yake binafsi, wazazi/walezi na Taifa kwa ujumla.

**MAHALI SHULE ILIPO.**

Shule ya Sekondari Mwalimu Nyerere ipo kata ya Segese katika Halmashauri ya Wilaya ya Msalala, Mkoa wa Shinyanga. Shule ina maabara nzuri kwa masomo ya sayansi, umeme, maji n.k. Shule ipo kilometa 40 kaskazini mwa mji wa Kahama katika barabara kuu iendayo mgodi wa dhahabu wa Bulyanhulu (TWIGA) na mkoa wa Geita. Upo usafiri wa magari makubwa (Mabasi) na madogo (Hiace) kutoka stendi kuu ya KAHAMA hadi SEGESE muda wote kuanzia saa 12 asubuhi hadi saa 12 jioni. Nauli kutoka KAHAMA hadi SEGESE ni sh. 3,000/=. Kwa wanafunzi

wanaotokea maeneo ya Mwanza, Mara, Bukoba na Geita kupitia Geita washukie kituo cha mabasi cha SEGESE, umbali kutoka hapo hadi mahali shule ilipo ni kilomita moja. Nauli kutoka GEITA hadi SEGESE ni sh. 7,000/=

Kwa Wanafunzi watokao Dar-es- Salaam, Morogoro, Dodoma wapande Magari yanayoenda Kahama, wakifika Kahama watapanda Mabasi yanayokuja Segese.

Kwa wanafunzi wanaotokea Tanga, Kilimanjaro, Arusha wapande basi za Moshi Geita au Arusha – Kahama watashukia Segese na kuripoti shuleni

**Karibu sana Mwl. Nyerere Sekondari.**

**……..………………**

**KAFURU SONGORA**

**MKUU WA SHULE**

**PAMOJA NA BARUA HII NAAMBATANISHA TAARIFA ZIFUATAZO:-**

1. Fomu na. 1 na 2 ambazo mnatakiwa mzijaze na kuja nazo shuleni .
2. Fomu na. 3 ambayo ataipeleka kwa Daktari wa serikali ili apimwe afya yake na ailete shuleni.
3. Nakala ya sheria na kanuni za shule ambazo atatakiwa kuzisoma, kuzielewa na kuzizingatia.
4. Lugha ya mawasiliano na taaluma shuleni ni KIINGEREZA tu.

5. **TAREHE YA KUFUNGUA SHULE**.

Shule itafunguliwa kwa muhula wa **kwanza mwezi wa saba tarehe ...............** Nafasi yako utakuwa umeipoteza mwenyewe kama hutaripoti mapema bila taarifa baada ya siku 30 tangu shule kufunguliwa.

## 2. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

### 2.1 SARE ZA SHULE (SCHOOL UNIFORMS)

**(**a) Shati tatu (3) nyeupe za tetron zenye mikono mirefu na collar na ziwe ndefu kwa ajili ya kuchomekea (anunue aje nazo shuleni)  Kwa waislam, rangi ya hijab (kijuba) ifanane na sare ya shule (yaani nyeupe).

(b) Sketi mbili (2) rangi ya Dark blue, Dark green(1) na light blue(1), ndefu .

(c) Viatu vyeusi jozi mbili vya ngozi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi (aje navyo).

(d) Soksi jozi mbili (2) nyeupe na ziwe ndefu (stocking) aje nazo.

(e) Sweater la kijani (dark green) mikono mirefu (aje nalo).

(f) Nguo za michezo : fulana ya bluu, bukta ya bluu, viatu vya michezo au raba na soksi rangi ya bluu ( aje nazo)

(g) Nembo mbili (2) kwa ajili ya masharti ya shule, Tishert mbili (2) Tai mbili (2) . Vifaa hivyo vinapatikana shuleni.

NB: Kama kiatu hakitakuwa cha kufunga kamba hakitakubaliwa

### 2.2 ADA NA MICHANGO YA SHULE

(a) Ada ya shule kwa mwaka ni Tsh. 70,000/= kwa mwanafunzi wa bweni, unaweza kulipa Tsh. 35,000/= kwa muhula au Tsh. 70,000/= kwa mwaka mzima katika muhula wa kwanza. Fedha hizo zilipwe kwenye akaunti ya shule namba **30601200118**, Jina la akaunti ni **SHULE YA SEKONDARI MWALIMU NYERERE** katika Benki ya **NMB**. Mwanafunzi anatakiwa kuja na stakabadhi original ya malipo (bank pay in slip) yenye jina lake aliyolipia benki.

**b) Michango inayotakiwa kulipwa na kila mzazi:-**

i. Shilingi 15,000/= kwa ajili ya ukarabati wa samani

ii. Shilingi 20,000/= kwa ajili ya taaluma

iii. Shilingi 6,000/= kwa ajili ya kitambulisho na picha

iv. Shilingi 30,000/= kwa ajili ya kuwalipa wapishi, walinzi na vibarua wengine

v. Shilingi **5,000/=** kwa ajili ya huduma ya kwanza, na Bima ya Afya (CHF) **sh. 6,000 - njoo na fedha taslimu**

vi. Shilingi 5,000/= kwa ajili ya tahadhari (fedha hii haitarejeshwa)

vii. Shilingi 10000 kwa ajili ya tai mbili(2). -**njoo na fedha taslimu**

viii. Shilingi 20,000 kwa ajili ya T-shirt mbili (2) za shule**.-njoo na fedha taslimu**

**Mbali na fedha taslimu,malipo mengine yote yaingizwe kwenye akaunti no: 30601200118 jina la akaunti ni SHULE YA SEKONDARI MWALIMU NYERERE katika benki ya NMB**

2.3 **VIFAA VYA USAFI**.

Mwanafunzi aje na vifaa vifuatavyo kwa ajili ya usafi:- (soft broom)

 Ndoo,beseni, fyekeo, reki, mfagio wa nje na wa ndani na jembe jipya lenye mpini

2.4 **VIFAA VYA BWENINI**.

Mwanafunzi aje na:-

i. .Shuka mbili (2) za rangi ya pinki, Blanketi moja, mto na chandarua.

ii. Dawa ya mswaki, miswaki, sabuni, taulo, kandambili, sabuni za kufulia na kuogea, mafuta, kiwi, brash na leso na Truck suit (rangi ya bluu).

iii. Locker au sanduku lolote imara kwa ajili ya kutunzia vitu vyake.

iv. Usihangaike kuja na godoro, godoro zinapatikana maeneo ya shuleni.

2.5 **VYOMBO VYA CHAKULA.** Aje na:-  Sahani, bakuli, kijiko, na kikombe

2.6 **VIFAA VYA DARASANI**. **Hakikisha Mwanao Anakuja Na Vifaa Vilivyo Orodheshwa Hapa Chini;-**

2.6.1 Madaftari 12 (counter book), Kalamu za wino, rula, na mathematical set.

2.6.2 Ream 1 ya karatasi (photocopy paper A4), (**ni lazima ikabidhiwe kwa msajili).**

2.6.3 Scientific calculator (fx: 982)

2.6.4 Mathematical table

2.6.5 Dissecting kit kwa wanafunzi wa Biolojia

2.6.6 Principle of Physics for class xi (2013) by chand's, S

2.6.7 Principle of Physics for class xii (2013) by chand's, S

2.6.8 Conceptual of chemistry for class xi (2013) by Dr. Sok. Jain

2.6.9 conceptual of Chemistry for class xii (2013) by Dr. S.K. Jain

2.6.10 Biological science (BS) 2017) by Green, Taylor & Staut

2.6.11A-level chemistry fourth edition (2014) E.N Ramsden

2.6.12Mathematics for class (ix & xii) (2012) by Chand's J.K Backhouse

2.6.13 Pure Mathematics 1 and 2 (1984)

2.6.14 Understanding Biology fourth edition by Green & Susan Toole

2.6.15 Biology for class xi & xii multi colour edition by S.Chand's

# SHULE YA SEKONDARI MWALIMU NYERERE

## FOMU NA. 1 – HATI YA KUKUBALI KUSOMA NA KUTOSHIRIKI KATIKA MGOMO, FUJO NA MAKOSA YA JINAI.

**NYONGEZA A: AHADI YA MWANAFUNZI**

Mimi ……………………………………………….. kutoka Shule ya Sekondari ……………………………

ninakubali nafasi hii niliyopewa ya kujiunga na kidato cha ……………… katika shule hii. Naahidi nitatimiza wajibu wangu kwa uwezo wangu wote na kwa manufaa ya Taifa letu kwa kufuata sheria, kanuni na taratibu za shule. Na kwamba nitakuwa mtiifu na sitashiriki katika vitendo viovu kwa muda wote nitakao kuwa hapa shuleni. Nikikiuka sheria, kanuni na taratibu za shule, niadhibiwe inavyostahili na hata kufukuzwa shule.

SAHIHI YA MWANAFUNZI ……………………………. TAREHE ……………………………..

**NYONGEZA B: AHADI YA MZAZI/MLEZI KUKUBALIANA NA SHERIA, KANUNI KULIPA MICHANGO YA SHULE NA MAELEKEZO MENGINE YA SHULE.**

Mimi ………………………………………………… ambaye ni *mzazi/mlezi wa mwanafunzi…………………………………………….. wa kidato cha ……………….. katika shule ya Sekondari Mwalimu Nyerere, ninakiri kukubaliana na sheria, kanuni kulipa gharama zote za shule pamoja na mahitaji mengine binafsi ya mwanafunzi kwa lengo la kumwezesha asome katika mazingira mazuri. Pia napenda kuthibitisha kwamba mtoto wangu hatachelewa shuleni kwa kukosa mahitaji kama ada, michango na mahitaji yake binafsi. Aidha ninaahidi kuwa ifikapo kila mwanzo wa muhula wa shule (mwezi Julai na Januari) nitakuwa nimemaliza kulipa gharama za shule kwa mujibu wa maelekezo yaliyotolewa hapo juu.

SAHIHI YA *MZAZI/MLEZI ………………………………… TAREHE ……………………………

NB: * Futa isiyohusika

**SHULE YA SEKONDARI MWALIMU NYERERE**

**S. L. P. 797, KAHAMA**

**FOMU NA. 2 – HABARI BINAFSI KUHUSU MWANAFUNZI**

1. Jina kamili la mwanafunzi …………………………………………………………………………………
2. Tarehe ya kuzaliwa ………………………………………………
3. Mahali alipozaliwa (wilaya) ……………………………. Mkoa ……………………………………
4. Jina la *Baba/mlezi ………..……………………………………………………………………………….
5. Mahali anapoishi sasa *Baba/mlezi (wilaya) ………………………. Mkoa ………………………….
6. Kazi ya *Baba/mlezi ………………………………………………………………………………….
7. Anwani ya *Baba/mlezi (S.L.P.)……………………………….. simu ……….……………………
8. Jina la *Mama/mlezi ………………………………………………………………………………...
9. Mahali anapoishi sasa *Mama/mlezi (wilaya) ………………………. Mkoa ………………………..
10. Kazi ya *Mama/mlezi ……………………………………………………………………………...
11. Anwani ya *Mama/mlezi (S.L.P) ……………………………….. simu ……………………………..
12. Dini ya mwanafunzi ………………………………………………………………………………...
13. Michezo anayoweza kushiriki mwanafunzi shuleni:

(i) …………………………………………………...

(ii) ……………………………………………………

(iii) ……………………………………………………

(iv) ……………………………………………………

(v) ……………………………………………………

14. Ndugu wa karibu watakaomtembelea mwanafunzi na uhusiano (mfano, baba,mama, mjomba, n.k)

a) Jina la ndugu …………………………………………….. uhusiano ………………………….

b) Jina la ndugu …………………………………………….. uhusiano ………………………….

c) Jina la ndugu …………………………………………….. uhusiano ………………………….

d) Jina la ndugu …………………………………………….. uhusiano ………………………….

- Tafadhali bandika picha zao hapa chini

**FORM NO. 3**

THE HEADMASTER,
MWL.NYERERE SEC.SCHOOL,
P.O.BOX 797,
KAHAMA.

**THE REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

TO THE MEDICAL OFFICER.……………………………………. ………………………………

**NAME OF STUDENT (IN FULL) ………………………………………………………………………**

Please, kindly I ask you to examine the student named above as to his/her physical and mental fitness for a fulltime study (two years course). The examination should include the following:

(a) Eye – sight

(b) Hearing

(c) Speech

(d) Limbs

(e) Chest

(f) Venereal diseases

(g) Epilepsy

(h) Leprosy

(i) Cirrhosis

(j) Other serious diseases

(k) Pregnancy

**MEDICAL CERTIFICATE PART A:**

(To be completed by Government Medical Officer) I have fully examined the above named person and consider that he/she is physically *FIT/UNFIT and mentally *FIT/UNFIT for a fulltime four/two years study/course. (a) Eye – Sight ……………………................

(b) Hearing …………………………………… (c) Speech ……………………………………. (d) Limbs …………………………………….. (e) Chest ………………………………………

(f) Venereal diseases …………………………

g. Epilepsy ………………………………….

h. Leprosy …………………………............

i. Neurosis ………………………………….

j. Cirrhosis ………………………………….

k. Other serious diseases ……………………

l. Pregnancy ………………………………..

# OFISI YA RAIS – TAMISEMI

HALMASHAURI YA WILAYA YA MSALALA

## SHULE YA SEKONDARI MWALIMU NYERERE

**S. L. P. 797, KAHAMA**

**SHERIA, KANUNI NA TARATIBU ZA SHULE.**

Shule ya Sekondari Mwalimu Nyerere inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978. Aidha shule hii inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara yenye dhamana ya Elimu nchini. Hivyo mara ufikapo hapa shuleni utatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo:-

A. Heshima kwa walimu, viongozi, wazazi, wafanyakazi wasio walimu na wanafunzi wenzako.

B. Kuhudhuria vizuri darasani na katika shughuli mbalimbali za ndani na nje ya shule.

C. Kuhudhuria masomo ya jioni (preparation).

D. Kuzingatia ratiba ya shule na ya bwenini.

E. Kuwa mahali unapotakiwa kwa wakati – kujali muda (mfano darasani, bwaloni, uwanjani, n.k.).

F. Kuvaa sare ya shule wakati wote uwapo ndani au nje ya eneo la shule.

G. Kuwa nadhifu (msafi) kimwili na mazingira ya shule wakati wote.

H. Kuwepo ndani ya eneo la shule wakati wote. Ni kosa kutoka ndani ya eneo la shule bila ruhusa.

I. Huruhusiwi kuja wala kuonekana na simu au vifaa vyake shuleni (mfano laini).

J. Huruhusiwi kulala bwenini wakati wa vipindi bila idhini ya Mwalimu wa Zamu. K. Ni kosa kuwa na mahusiano ya kimapenzi na mtu yeyote.

**MAKOSA YAFUATAYO ADHABU YAKE NI KUFUKUZWA SHULE.**


1. Wizi wa aina yoyote..
2. Uasherati, ushoga, usagaji na ubakaji.
3. Ulevi wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya.
4. Kumiliki/kuwa na simu shuleni.
5. Kupiga,kupigana, ugomvi na kutumia lugha chafu kwa viongozi au wenzako.
6. Kupata mimba na kutoa mimba ndani na nje ya eneo la shule.
7. Kujaribu, kusababisha, kuongoza au kushiriki kugoma na kuvuruga amani/usalama.
8. Kuolewa au kuoa.
9. Kukataa adhabu kwa makusudi.
10. Kuharibu kwa makusudi mali ya shule.
11. Makosa ya jinai, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.

12. Kudharau Bendera ya Taifa, Wimbo wa Taifa, Fedha za Taifa, na nembo ya Taifa.
13. Kuonekana kwenye vilabu vya pombe, bar, kumbi za starehe na nyumba za kulala wageni.
14. Kutoka nje ya mipaka ya shule bila idhini ya mwalimu.
15. Kutohudhuria nywele kwa mtindo usiokubalika masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro
16. Kusuka. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa kutoka usoni kwenda kisogoni. Nywele zisisukwe kwa kutumia nyuzi au rasta.
17. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule
18. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu, n.k.

**PICHA YA MSHONO WA SKETI**



KARIBU SANA KATIKA SHULE YA SEKONDARI MWALIMU NYERERE



…………………………..
KAFURU M. SONGORA.
**MKUU WA SHULE.**